# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI

**09 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

### KIKAO CHA AROBAINI NA MBILI - TAREHE 09 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Maelezo ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ARDHI, MALIASILI NA UTALII:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025].*

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**533 MHESHIMIWA MINZA SIMON MJIKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuhakikisha inawawezesha kiuchumi Watu wenye Ulemavu.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**534 MHESHIMIWA JAFARI WAMBURA CHEGE (RORYA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini ujenzi wa Kituo cha Afya Rabour - Rorya utakamilika.

**535 MHESHIMIWA SELEMANI JUMANNE ZEDI (BUKENE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamaliza tatizo la upungufu wa Watumishi wa Kada ya Afya - Bukene.

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

**536 MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga ukuta eneo la Pwani ya Mji wa Kilwa Kivinje ili kuzuia maji ya Bahari yanayoathiri Wananchi.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**537 MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali italeta Marekebisho ya Sheria ya Ndoa kuhusu ndoa za jinsia moja au Muswada wa Sheria kupiga marufuku ndoa za jinsia moja.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**538 MHESHIMIWA FRANCIS KUMBA NDULANE (KILWA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Kilwa.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**539 MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itakamilisha zoezi la upimaji wa ardhi katika Halmashauri ya Kasulu DC.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**540 MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itawapa makoti ya kujikinga na baridi Askari Polisi wanaofanya kazi katika Mkoa wa Mbeya.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**541 MHESHIMIWA ABEID IGHONDO RAMADHANI (SINGIDA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa Wakulima ili kuondoa changamoto zilizopo - Singida Kaskazini.

**WIZARA YA KILIMO:**

**542 MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali haioni ipo haja ya kupitia upya Mikataba ya Mashamba ya Ushirika na kufanya tathmini ya ardhi ya mashamba hayo.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**543 MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka huduma ya bure ya mtandao kwenye Vyuo na Shule zote nchini.

**WIZARA YA UJENZI:**

**544 MHESHIMIWA ISSA JUMANNE MTEMVU (KIBAMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya kutoka Makondeko - Kwembe hadi Mloganzila.

**545 MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Mshauri Elekezi atatangazwa kuanza upembuzi yakinifu Barabara ya Kahama, Kharumwa, Nyang'hwale - Busisi ambayo ni ya muda mrefu.

**546 MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Wasso hadi Loliondo Km 10 utaanza.

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Shirika la Nyumba la Taifa wa Mwaka 2025 *[The National Housing Corporation (Amendment) Bill, 2025].*

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **09 JUNI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |